# NI WAKATI WA MAVUNO

*Mt. Yohana 4:35 Inueni macho yenu myatazame mashamba,ya kuwa yamekwisha kuwa meupe,tayari kwa mavuno.*

Sikiliza kile nabii wa Mungu alichosema juu ya hilo**:**

Ile siri ya magugu na ngano ya Matayo 13:24-30,sasa hivi nayo Imetimizwa.

Akawatolea mfano mwingine,akisema,ufalme wa Mbinguni umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema katika konde lake; lakini watu walipolala akaja adui yake akapanda magugu, katikati ya ngano,akaenda zake**.**Baadaye majani ya ngano yalipomea na kuzaa,yakaonekana na magugu.Watumwa wa mwenye nyumba wakaenda wakamwambia,bwana hukupanda mbegu njema katika konde lako? limepata wapi basi magugu? akawaambia,adui ndiye aliyetenda hivi, watumwa wakamwambia basi wataka twende tukayakusanye? akasema, la;msije mkayakusanya magugu,na kuzing`oa ngano pamoja nayo;viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno;na wakati wa mavuno nitawaambia wavunao,yakusanyeni kwanza magugu,myafunge matita matita mkayachome; bali ngano ikusanyeni ghalani mwangu.

Ile ngano na magugu,ambayo ilikuwa pamoja kutoka wakati wa kwanza mpaka sasa,vinavunwa. kile ambacho nikea ilikusudia kukamilisha mwisho wake kimetimia**.**zikitumia nguvu zote za madhehebu,kanisa la uongo linageuka kutoka kwenye kila chembe ya ukweli na kwa nguvu za siasa linajiimarisha lenyewe likiungwa mkono na serikali nalo linaweka utaratibu wa kuwaangamiza/kuwatokomeza kabisa waaminio wa kweli.Lakini pale linapokuwa tayari kukamilisha mpango wake woga kiwaoga, ile ngano inakusanywa ghalani.

Huu wakati ndio wakati wa mwisho wa nyakati saba za kanisa.kile kilichoaza katika wakati wa kwanza au wakati wa Efeso ni lazima kitakuja kwenye ukamilifu wa matunda na kuvunwa katika wakati wa mwisho au wakati wa Laodikia.Ile mizabibu miwili itazaa matunda yao ya mwisho.zile roho mbili zitakoma katika udhihirisho wa kila moja katika ule ukomo wa mwisho wao**.**Kule kupanda, kumwagilia/kumwesha, kule kukuwa kunafikia ukomo.wakati wa mchipuko unakoma.na lile mundu la kuvunia unavuna mavuno.

Maneno ya Yohana mbatizaji ambayo kwa usahihi kabisa aliweka uhusianowa Kristo na lile kanisa la kweli na la uongo sasa unatimia (Matayo3:11-12).

Kristo, yule mvunaji mkuu, sasa hivi anavuna mavuno ya nchi (dunia) anakusanya ngano na kuiweka kwenye ghala kwa kuwafia walio wake na kuwachukuwa milele na kuwa nao Yeye.halafu anarudi na kuwaangamiza waovu kwa moto usiozimika.

Na sasa tunakuja kwenye wakati wa mwisho;wakati wa laodikia.huo ndio wakati wetu.tunajua ni wakati wa mwisho kwa maana Wayahudi wamerudi wako Palestina .haijalishi wamefikaje pale;wako pale.na huu ni wakati wa mavuno,lakini kabla ya kuwepo wakati wa mavuno, lazima uwepo wakati wa kuivisha,na wa kukomaa kwa mizabibu yote miwili.

Wakati wa Lutherani,ulikuwa wa kuchipua,wakati wa Wesley ulikuwa wakati wa kukuza.wakati wa Laodikia ni wakati wa kuvuna wa kukusanya magugu kwa ajili ya kufungwa na kuchomwa; na kuweka ghalani ngano kwa ajili ya Bwana(Matayo 13:36-43) wakati wa kuvuna;je uliona kuwa wakati wa kuvuna, ingawa kuna kule kuharakisha kuiva,baadaye kuna kule kukuwa taratibu sana mpaka inafikia hakuna kukua tena? Je hicho sicho kitu tunachokiona hasa leo?ule mzabibu wa uongo unapoteza wengi sana wakienda kwenye ukomunisti,na aina nyingine za imani.idadi ya watu haiongezeki kama ambavyo wangetutaka sisi tufikiri/tuamini.Ile nguvu yake ya kushikilia watu sio kama ilivyokuwa zamani,na mara nyingi kwenda kanisani ni kutaka tu kuonekana. Na mzabibu wa kweli nao? Vipi kuhusu huo? Je idadi ya watu imeongezeka? iko wapi ile idadi kubwa ya watu iliyokuwa inakuja kwenye uamsho na kujibu wito wa madhabahuni?wengi wao ni hali ya msisimko tu katika kumkaribia kwao.au shauku yao ni kitu Fulani cha kuonekana badala ya shauku ya kile ambacho ni cha kiroho? Huu wakati sio kama wakati wa Nuhu alipoingia kwenye safina, na mlango ulifungwa, lakini Mungu alivuta subira ya hukumu kwa siku saba? (mwanzo 7:1-10) hakuna hata aliyemgeukia Mungu katika hizo sikusaba za ukimya.na bado ni wakati wa mavuno.hapo basi lazima waje katika uwanja katika wakati huu wa mwisho wale ambao wataifanya ngano na magugu vikomae. Yale magugu tayari yanakomaa haraka sana chini ya walimu wapotoshaji ambao wanawageuza mbali na Neno (Waefeso4:11-

16).Lakini ngano nayo lazima ikomae.Na kwake huyo Bibi arusi,Mungu anamtuma mjumbe-nabii pamoja na huduma iliyo thibitishwa ili aweze kukubaliwa na wateule (malaki 4:5-6) watamsikia yeye kama vile kanisa la kwanza walivyomsikiliza Paulo,na yeye atakomea katika Neno mpaka awe bibi arusi Neno-na zile nguvu na uweza wa kiutendaji wa Mungu utaonekana kwake ambavyo siku zote hutokea katika Neno na imani isiyoghoshiwa (Yohana 14:12) mvua za vuli zitakuja tu baada ya mvua za masika ambazo ni mlipuko au mvua za mafundisho.mvua za vuli (baadaye),ni mvua za mavuno**.** [1]

Maisha yoyote unayoishi,hivyo ndivyo maisha yoyote utakayovuna.kama vile upandavyo,unavuna (Gal6:7-10) Mungu ameniruhusu kuishi muda wa kutosha kuona hilo,kuwa huwezi kutenda kosa na kuacha vivi hivi tu,inakupasa ufanye kitu ambacho ni sahihi,kwa sababu Kristo amefufushwa kutoka kwa wafu,na macho yake yanaliangalia kanisa,na analiangalia hilo na kuliongoza.kamwe asitende kinyume na vile Roho Mtakatifu apendavyo,akikuambia ufanye kitu Fulani (Efeso4:30)Haijalishi dunia inasemaje,wewe fanya yeye asemavyo ufanye.siku zote yeye atauthibitisha ukwelina kuuweka ukweli ulionyooka.[2]

"Hiki ndicho ninachojaribu kuwaambia ninyi,sheria ya uzazi ni kuwa kila mbegu aina izae kwa jinsi yake,kama ilivyo katika kutoka1:11-12, na Mungu anasema,ichi na itoe majani, mche utoao mbegu,na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi yake,juu ya nchi;ikawa hivyo"uhai wowote uliokuwa ndani ya mbegu ulidhihirika kuwa mmea na hatimaye matunda.sheria hiyohiyo inaihusu kanisa leo.mbegu iwayo yote iliyoanzisha kanisa itadhihirika na itakuwa kama ile mbegu ya mwanzo kwa sababu ni mbegu ile ile**.** Katika siku hizi za mwisho yule Bibi arusi wa Kweli (mbegu ya Kristo) itafikia lile jiwe la kifuniko,na hilo litakuwa kanisa tukufu,uzao wa kifalme,kadiri wanavyomkaribia Yeye.wao walio Bibi arusi watafanana sana naye kiasi kwamba wataichukuwa sura yake hasa (Efeso5:25-27) hii ni kwa kusudi la kuungana naye.watakuwa mmoja.watakuwa udhihirisho halisi wa Neno la Mungu aliye hai.madhehebu hayawezi kuzaa hiyo.(mbegu potovu)watazaa kanuni zao na maungamo,vikiwa vimechanganywa na neno.huu mchanganyiko unaleta mbegu ya haibrid.[3]

Namkumbuke,wakristo marafiki mimi ni mwanadamu,naweza kufanya makosa lakini Mungu,akiwa Mungu hawezi kufanya makosa.maandiko yote yaliyoandikwa lazima yatimie.Yesu alisema hivyo.kwa hiyo tunayo mambo hapa kwenye maandiko ambayo ni lazima yatimizwe.na hilo ni moja la mabo hayo, kule kususiwa kunakuja(Ufunuo13:11-18)lakini kabla ya kususiwa huko na kuwekewa alama ya mnyama,lazima kuwe na mbegu iliyopandwa kwa ajili ya Munguili aliondoe kanisa kati yake.unaelewa sasa mbegu lazima zipandwe.mbegu ya kidhehebu kufanya mfano wa au sanam ya mnyama,kanisa la Roma……na pale lazima awepo Bibi Arusi wa kweli.

Sasa,kumekuwa na mbegu za aina tatu tofauti zilizopandwa:ya kidhehebu:Bill Graham;alikuwa ndiye kiongozi wa kupanda,OralRoberts kwa wapentekoste----mbegu ya kipentekoste imekwisha pandwa.(ninazungumzia juu ya madhehebu sasa) na halafu neno pia limepandwa.sasa inabidi muelewe ndugu, silisemi hili tena labda Mungu aniambie mimi.nataka mlipate hili vizuri na wazi.mbegu aina tatu zimepandwa.hiyo ndiyo ule upandaji unaelekea mwisho.mbegu inabidi zipandwe kabla ya mvua kunyesha(hiyo ni sawa )au kwa namna nyingine Roho.sasa,mnaweza msikubaliane pale.lakini shikilia hapo kwa dakika, mbegu lazima zipandwe na halafu mvuainyeshe kumwagilia mbegu maji. Hiyo nisawa[4]

Kama tunapanda mbegu za kidhehebu,tutavuna mavuno ya kidhehebu,hiyo ni sawa kabisa. Hivyo ndivyo tulivyofanya

Kama ukiangalia lile Neno katika kiebrania mvua za kwanza na za mwisho; mvua za kwanza inamaanisha mvua za kupandia.na halafu sasa Roho anaposhuka wenye haki na wasio haki.kama tulipanda mbegu ya kidhehebu,tutavuna mbegu ya kidhehebu katika mavuno.[5]

Mbegu ya kidhehebu hutoa msamaha wa kidhehebu hiyo ni sahihi kabisa.Mungu alisema,``Neno lizae kwa jinsi yake"na hivyo ndivyo ilivyo.hiyo ni sawa**.**Oh ndugu,maandiko ni kweli unaamini hilo? [4]

Tunaona kuwa wa kwanza kupanda mbegu za hitilafu alipewa jina la shetani,na tunajua ilikuwa ni mwanzo 1.Pale tunaona hilo, na hapa katika kitabu cha Matayo 13,Yesu bado anaita kila aina la hitilafu kwenye Neno lake ni shetani.chochote kipandacho mbegu ya hitilafu,kinyume na Neno la Mungu lililoandikwa,au kuweka tafsiri ya apendavyo mtu, ni mbegu ya hitilafu.Mungu hataliheshimu hilo**.** [6]

Jambo moja Mungu analichukia ni kupanda mbegu ya hitilafu miongoni mwa ndugu[7] huwezi hilo. Haiwezi kuchanganyika hakika haiwezi ni kama mbegu ya haradali(Matayo 17:20);haingeweza kuchanganyika na kitu kingine;huwezi ukaichanganya;lazima iwe kitu halisi mbegu ya hitilafu---[6]

Unaona,tupa mkate wako juu ya maji,utakurudia siku moja. Panda mbegu sahihi, utavuna mavuno sahihi.Kama ukipanda mbegu zisizo sahihi,utavuna kitu ambacho siyo sahihi.Huwezi ukaenda mashariki na magharibi kwa wakati mmoja,inabidi uende upande mmoja au upande mwingine.fuata dira,na dira ni Roho mtakatifu.Ile sumaku ya kaskazini unashikilia ile dira hasa kaskazini.Je hiyo siyo ajabu iliyo eletroniki ya hewa---[8]

Je Yesu hakusema kuwa mpandaji alipanda mbegu na nyingine zikaangukia njiani na ndege wakazila hizo? Nyingine ziliangukia kwenye miamba na utajiri wa dunia ukazisonga, na kadhalika.Na je hakusema nyingine zilizaa mara mia? (Matayo13:1-9,18-23,36-43).unaona,inabidi kwanza uliruhusu Neno liangukie katika aina ya imani iliyo nzuri.na halafu sasa hiyo imani inazaa kile ambacho Neno limesema, kwasababu neno ni mbegu(Luka 8:11). Neno la Mungu,hapa hapa,ni mbegu ambayo mpanzi alipanda. Na kila mbegu itazaa kwa aina yake kama imewekwa katika mazingira mazuri na hali nzuri.[9]

Sasa, Yeye ameahidi kukupelekea nuru ya mbinguni (Zakaria 14:6-7) kuivisha ile mbegu Neno ambayo itapandwa kwa ajili ya siku ya leo.Ile mbegu iko hapa,ile mbegu ni Biblia kwanini? Yesu alisema hivyo, “lile Neno ni mbegu ambayo mpandaji alipanda” na sasa, kabla hujawa na mzao yoyote, haijalishi kama ulipanda mbegu, lazima ipate nuru iweze kuivisha mbegu, au itaoza na haitakuwa nzuri, itapotea,lakini kama ina mbgu katika ardhi,udongo sahihi na mwanga sahihi wa jua juu yake,lazima itaiva.Na yeye ameahidi hilo katika siku za mwisho,katika wakati wa jioni (nuru) itakuja kuivisha ile mbegu.Ile mbegu inahubiriwa mwana wa Mungu anaivisha mbegu kwa kuthibitisha(Neno)hilo,akiifanya izidi kukuwa miongoni mwenu na kuthibitisha kuwa ni kweli[10]

Kwa hiyo mbegu ya adui iliendelea mbele,yule mpandaji mwema aliendelea kupanda mbegu nzuri,na adui akaja nyuma yake na kupanda mbegu potovu.Lakini mvua hunyeshea wema na waovu (Matayo,5:45) vyote lazima vikue.

Yesu alisema. “viache vikue pamoja,katika siku ile vitafungwa pamoja”yale magugu (Matayo 13:30) .na wanayafunga pamoja sasa,katika madhehebu yakiendelea kufungwa katika fungu kubwa;Baraza la makanisa duniani.na mwisho ni nini? Ni kuchomwa moto (ufunuo18:8-10).Lakini ngano inachukuliwa ghalani (2Wathesalonike2:7-12). Unaona? pale wote wanaishi kwa kitu kile kile,maji yale yale mvua ile ile---[11]

Najua ninazunguka na kuchukuwa muda mrefu,lakini nilitamani kuwaletea picha hii kwenu, ili msije kamwe kuisahau hiyo.haijalishi uko mahali gani.kama uko katika dimbwi la kuogelea,kama uko kwenye hilo wanalopigia kamari, kuna mtu asiyeonekana anakuangalia wewekwama unastahimili mashutumu kwa ajili ya jina la Bwana,haijalishi ninini,muweke alama yoyote utakaye,na uone,yule mtu anavuna anacho panda wakati wote.kama anafanya jambo lililo sahihi,atakuja utukufuni na hilo.Huwezi ukalishinda hilo ni Mungu.yuko hapa.Anajua kilindi hasa cha moyo wako. Anajua wewe ni nani na vyote ulivyofanya.[12]

“ Mungu hadhihakiwi.chochote mtu apandacho,hicho ndicho atakachovuna”Hawawezi kudhihaki na kuchekelea, na kuendelea tu hivyo.kama vile mkate katika maji.utakurudia(Mhubiri 11:1) [13]Neno la Mungu kila wakati lazima litimizwe.lile gurudumu la Mungu la unabii linazunguka taratibu,ila ni kwa uhakika kama unafanya makosa,na unafikiri utaachwa tu.lakini kumbuka,kijana mdogo mvulana au msichana, siku moja litazungukia hapo mlangoni kwako.Utashangaa ni lini na ni nani kwa namna gani, lakini litakufikia tu.kila wakati utavuna ulichopanda.Mungu amesema hivyo.lazima itakuwa hivyo.kwamba neno la Mungu limesimama imara mbinguni na hata milele”(zaburi 119:89) Limekwisha kunenwa pale hawabishani nalo; tayari linasimama. Tuna bishana juu yake. Lakini utukufu lina simama. Mungu anaposema kitu chochote lazima kiwe hivyo. Vema. Je,hiyo si ajabu? [14]

Sasa, unaweza kufanya makosa, na kila wakati ulifanya chochote kimakosa, utaenda kulipia kwa ajili ya hilo. Ndiyo bwana, utavuna kile upandacho. Lakini hilo halina uhusiano wowote na wokovu wako. Unapokuwa umezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu (Yohana3:3-8),unao uzima wa milele na huwezi kufa tena kama vile Mungu asivyoweza kufa (Yoh 5:24)we ni sehemu ya Mungu;ni mwana wa Mungu [15]

Hivyo Kristo alikuwa uzao wa Ibrahimu,na sisi tukiwa tumekufa ndani ya Kristo na kubazinzwa katika mwili wake,sisi ni uzao wa Ibrahimu na tu warithi wa ahadi (Galatia 3:29).utaweza vipi kuanguka,kama Mungu amekupa wewe ahadi?utawezaje kurudi nyuma, na kwenda mbali,na kwenda kuzimu kwa ajili ya hilo?

Sasa, unasema, "vema hatuwezi kurudi nyuma?" hakika unaweza.na unaporudi nyuma,utaenda kuadhibiwa na usiwe na wasiwasi,Ibrahimu aliadhibiwa,nawe utaadhibiwa(Mwanzo 20).usifikirie inakupa haki ya kutenda dhambi.haikupi. utalipia kwa kila kitu ufanyacho unavuna kile ufanyacho. Utavuna kile upandacho.unatenda dhambi ndogo, nawe utavuna karai la kufulia lililojaa.Hiyo ni kweli.Lakini ndugu,hilo halimaanishi kusema kuwa umepotea.hiyo ni sahihi kabisa.Ibrahimu alivuna hasa kile alichopanda.hiyo ni kweli,lakini alikuwa bado ameokoka.

Lile agano Mungu alilowena na Waisrael,Israel walipoteza urithi wao; walipoteza nchi yao ya ahadi.na wakaenda kuishi Misri. Lakini hawakupoteza Agano lao. Mungu alisema, Ninakumbuka ahadi yangu kwa Ibrahimu. Ninaikumbuka, nami nimeshuka chini kuwaokoa watu wangu. (Kutoka3,6:2-5) Nenda kule chini Musa na Umuambie Farao, Awaachie watu wangu watoke Ninakumbuka niliweka ahadi na Ibrahimuna uzao wake"[16]

Sasa, wanapata mapigo kwa kufanya yasiyo sahihi. Unavuna unachopanda; unapata hilo, usifikiri sasa unaweza ukaenda nje nakutenda dhambi na uachiliwe**.** Kama unafanya hivyo namtazamo huo, inaonyesha kamwe hujazaliwa mara ya pili, unalipata hilo? Kama bado unayo shauku ndani yako yakutenda yasiofaa, hapobasi bado uko makosani (Waebrania10:2) Unaona? Kwa maana amewakamilisha milele waleambao…(Waebrani10:14) Na hawa wanyama chini ya Agano la kale, wakati wa siku za sheria, walitoa sadaka kila mwaka, kuendelea hazingeweza kuondoa dhambi. Lakini tunapoweka mikono yetu juu ya kichwa chake na kukiri dhambi zetu na tumezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu,hatuna tena shauku ya kutenda dhambi(1Yoh5:18) dhambi imepita kutoka kwako hilo ni kwa muda wa milele yote [17]

Lakini ngojea nikuambie kitu Fulani; tunahitaji kitu cha kutuchemsha,hili taifa linahitaji mambo tuliyokuwa nayo mwanzoni;tumeyapotezatunajaribu kuishi kwa sifa ambazo mwingine alizifanya.Tutavuna kwa ajili ya hao.Mungu aliwafanya Israel kwa jinsi ya moyo wake,aliwafanya wavune, na sisi tutavuna pia ,kwa yale tufanyayohatuna tu kingine mbele yetu ila ni kuvuna,tumevuka mstari wa neema na huruma, na hakuna kilichobakia ila kuvuna.Wekea hilo alama katika bablia yako.Mimi ni mzeee,kweli.Napengine nitakapokuwa nimeondoka,na kuendelea na kuendelea, utakuja kuona hayo maneno ni ya kweli.tutaenda kulipia.Tumepimwa katika mizani na tumeonekana tumepungua,na hatuna njia ya kuponea.Hakika.tayari tumevuka huo mstari. Inabidi uvune kile ulichopanda kila wakati**.** [18]

Na hakuna mmoja anayejua jinsi nilipendavyo hili taifa.lakini angalia, ndugu yangu,Israeli pia walichaguliwa na Mungu,na amewatuma manabii wake na watu wakuu.lakini Mungu hawezi kuvumilia dhambi.aliwafanya Israeli wavune kila mbegu waliyopanda.na kama aliwafanya Israel wavune, atatufanya na sisi tuvune kile tulichopanda.Yeye haangalii uso wa mwanadamu**.**(Wakolosai3:25,1Petro1:17). [19]

Mungu anachukia dhambi,na dhambi lazima ihukumiwe.ilikuwa imesemwa kwamba kama Mungu hataihukumu Amerika mapema kwa dhambi zake.anapaswa kuwa fufua Sodoma na Gomora na kuwaomba msamaha. Hakika.na tunavuna tulichopanda,na kila mmoja ambaye anakitu cha rohoni ndani yake anafahamu kuwa hiyo ni kweli.tuko mwisho wa njia. [20]

Tunaliangalia hilo hatujui hilo litakuwa wakati gani.ninaamini ni wakati huu,na ninataka nishikilie tochi niiwashe.Na sikiliza sasa, lipate hili kwa usahihi.nataka niishi kila muda wa maisha yangu kwamba ninamtarajia yeye muda unaofuata,lakini nataka niendelee kana kwamba itakuwa miaka elfu kumi kuanzia sasa.bado ninahitaji kupanda mbegu,kuvuna mavuno nataka nihubiri injili na kuendelea na shughuli kama siku zote nilivyofanya. Niendelee kama hivyo, macho yangu yakiangalia juu,nikikesha, nikiendelea kukusanya miganda mizuri, ile mbegu.halafu mwaka ujao nitapanda mazao yangu tena, "Bwana nilitegemea utakuja mwaka uliopita,lakini kwa vile hukuja,pengine utakuja mwaka huu.kwa hiyo nitapanda mazao yangu na kulea watoto wangu,kama utakawia watakuwa na kitu Fulani cha kula; kama hutakawia, nitakuwa ninakungojea" unaona ilivyo? Endelea mbele na shughuli zako kama kawaida**.** [21]

Nukuu za kiingereza**:**

1**.**Wakati wa kanisa wa Laodikia, kitabu cha nyakati saba uk 361-362/375/377.

2. Mtetezi wangu anaishi (55-04105)Aya77
3. Wakati wa PergamoKNS za kanisa uk.171
4. Lile Neno lililonenwa ndiyo mbegu ya asili(62-0318).Aya126/111/44
5. Msikieni Yeye(62-0711) Aya 50
6. Mbegu ya hitilafu"(65-0118),Aya31
7. Wakati wa kanisa la Filadefia Aya31
8. Kwa nini watu wanayumbishwa huku na huko (56-0101) uk 8
9. "Malkia wa sheba"(61-0219),Aya 33
10. "kutambua siku yako"(64-0726M) Aya 195
11. "Makao ya baadaye (64-0802)uk 48
12. "Ushirika ni kwa ukombozi"(55-0403),Aya 124
13. Mungu wa wakati huu mwovu(65-0801m),Aya 168
14. "Israel pale kwenye bahari ya shamu?"53-0327 Aya 34
15. Nafasi ndani ya Kristo(600522m) Aya 36
16. Waebrania sura ya 6 (57-0908E) uk.232
17. Waebrania sura 687(57-0915M) uk264
18. Ushawishi (64-0315) Aya 23
19. Uwe na hakika na Mungu(64-0315) Aya 15
20. Njoo haraha kimbilia huku (58-0202),Aya 17
21. Maswali na majibu(62-0527) COD uk 715

*jiwe la kiroho la kujengea na 103. kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de*

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*
*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*
*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0713230098*